



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI

MSIMAMIZI WA UCHAGUZI

HALMASHAURI YA SHINYANGA MANISPAA

JIMBO LA SHINYANGA MJINI



Kumb. Na. ....

Tarehe 07.12.2022

**TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI ZA MUDA**

Msimamizi wa Uchaguzi Jimbo la Shinyanga Mjini kwa kuzingatia kanuni ya 12 ya Kanuni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa (Uchaguzi wa Madiwani) za mwaka 2020, anakaribisha maombi kutoka kwa Watanzania wenye sifa na uwezo wa kujaza nafasi za Watendaji wa Uchaguzi utakaofanyika tarehe 17 Disemba, 2022 katika Kata ya Mwamalili kama ifuatavyo: -

1. MSIMAMIZI WA KITUO CHA KUPIGIA KURA (NAFASI 13).
  2. MSIMAMIZI MSAIDIZI WA KITUO CHA KUPIGIA KURA (NAFASI 24).
  3. KARANI MWONGOZAJI WAPIGA KURA (NAFASI 13).
- A. **SIFA ZA WAOMBAJI WA NAFASI YA MSIMAMIZI AU MSIMAMIZI MSAIDIZI WA KITUO CHA KUPIGIA KURA**
- (a) Awe raia wa Tanzania mwenye umri wa miaka 18 au zaidi;
  - (b) Asiwe shabiki au kiongozi wa chama cha siasa;
  - (c) Awe mwadilifu, mtiifu na mwenye akili timamu;
  - (d) Awe amemaliza elimu ya kidato cha nne (4) au zaidi na anaweza kusoma na kuandika vizuri. Pia, anayeweza kuyaelewa Maelekezo ya Wasimamizi wa Vituo vya Kupigia Kura; na
  - (e) Ikiwezekana awe mkazi wa kata ambayo anaomba kufanya kazi.
- B. **SIFA ZA WAOMBAJI WA NAFASI YA KARANI MWONGOZAJI WA WAPIGA KURA**
- (a) Awe raia wa Tanzania mwenye umri wa miaka 18 au zaidi;
  - (b) Awe mkazi wa kata ambayo atafanyia kazi ya kuongoza wapiga kura;
  - (c) Ikiwezekana awe mpiga kura wa kituo anachofanyia kazi;
  - (d) Awe mwadilifu, mtiifu na mwenye akili timamu;
  - (e) Awe na elimu isiyopungua kidato cha nne na anayeweza kusoma na kuyaelewa Maelekezo kwa Makarani Waongozaji Wapiga Kura; na
  - (f) Asiwe shabiki au kiongozi wa chama cha siasa.
- C. **MALIPO**

Malipo yatakuwa kama ifuatavyo: -


- i. Msimamizi wa Kituo siku ya Uchaguzi atalipwa posho ya Tzs. 60,000 kwa siku kwa muda wa siku mbili, posho ya chakula Tzs 10,000 kwa siku moja na nauli Tzs 20,000;
- ii. Msimamizi Msaidizi wa Kituo atalipwa posho ya Tzs. 50,000 kwa siku kwa muda wa siku mbili, posho ya chakula Tzs 10,000 na nauli Tzs 20,000; na
- iii. Karani Mwongozaji Wapiga Kura atalipwa posho ya Tzs 50,000 kwa siku moja na posho ya chakula Tzs 10,000.

**D. MASHARTI YA JUMLA KWA KAZI ZOTE.**

- i. Waombaji waambatishe maelezo binafsi yaliyojitosheleza (Detailed C.V) yenye anuani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya wadhamini (Referees) wawili.
  - ii. Maombi yote yaambatane na Vyeti vya taaluma, nakala za Vyeti vya Kidato cha Nne, Kidato cha Sita au kuhitimu mafunzo kwa kuzingatia sifa alizonazo kwa mujibu wa Tangazo hili.
  - iii. Waombaji waambatishe picha mbili 'Passport size' za hivi karibuni.
  - iv. Waombaji ambao ni Watumishi wa Umma wapitishe barua zao za maombi ya nafasi za kazi kwa waajiri wao.
  - v. Waombaji watakaowasilisha taarifa na sifa za kugushi watachukuliwa hatua za kisheria endapo watabainika.
- Mwisho wa kutuma na kupokea maombi ya kazi ni tarehe 07 Disemba, 2022. (Mwisho TAR. 9/12/2022).

Anuani ya kutuma maombi ya kazi ni: -

Msimamizi wa Uchaguzi,  
Jimbo la Shinyanga Mjini,  
S. L. P 28,  
SHINYANGA

  
MSIMAMIZI WA UCHAGUZI  
JIMBO LA SHINYANGA MJINI

MSIMAMIZI WA UCHAGUZI  
JIMBO LA SHINYANGA MJINI

NB. MAOMBI YOTE APELEKWE OFISI YA KATA YA  
MWAHALILI